

# SULUHISHO LA MTU ASIPOE KIROHO AU KUONDOKANA NA ROHO

## YA WOGA NI KUJAZWA ROHO MTAKATIFU.

### MAANDIKO: MDO 1:4,8, 2:1-4, 14-16, 22-24,29,37-43

#### 1. UTANGULIZI

Sote tumesoma maisha ya Mtume Petro tangu Yesu alipomwita akiwa mvuvi, jinsi Yesu alivyompenda na kujidhihirisha kwake mara nyingi inawezekana kuliko kwa wanafunzi wengine wote, pamoja na Yesu kufanya haya yote kwa Petro; bado tunaona jinsi Petro alivyomkana Yesu na kutishwa hata na kijakazi na baadaye kumwacha Yesu na kurudia kazi yake ya uvuvi hadi Yesu alipomwende huko na kujidhihirisha kwake na kumwita tena kwa mara ya pili ili alishe pamoja na kuchunga kondoo wa Bwana. Katika matendo sura ya pili tunamwona Petro wa tofauti sana baada ya kujazwa na Roho Mtakatifu, Petro ambaye anasimama katikati ya upinzani bila woga wa aina yoyote na kuwataka wanaume wamsikilize akinena habari za Yesu Kristo na kuwakemea na baadaye anawaambia yawapasayo kutenda na watu zaidi ya **3000** wanaokoka siku moja na anawaelekeza wakabatizwe!! Nini suluhisho la kiroho chake, nini lilikuwa suluhisho la roho ya woga alivyokuwa nayo Petro!!

#### **“Kujazwa na Roho Mtakatifu**

2. Paulo alilijua sana jambo hili, maana yeye alipokutana na Yesu njia na kugeuzwa nia yake aliyokuwa nayo kinyume na Kanisa la kwanza, pamoja na kuchukuliwa hadi mbinguni ya tatu na kuona mengi na kufahamu mengi, sharti lake la kwanza kabla ya kuanza kutumika na kumshuhudia Yesu kwa Wafalme na Mataifa kama wito wake ulivyokuwa, alijazwa Roho Mtakatifu kwanza **Mdo 9:17-19, 13:9-12**. Roho Mtakatifu alikuwa suluhisho la hali ya juu sana kwa Paulo na mwalimu wake wa hali ya juu sana kiasi Paulo hakuogopa kufa tena.

- **Moja wapo ya kazi tatu muhimu sana za Roho Mtakatifu ndani ya mwamini ni;**

a. **Kuimarisha kabisa utu wake wa ndani Efes 3:14-16**( Hata gari ambayo injini yake ni nzima inapanda kila aina ya milima bila shida yoyote. Kwa maana nyingine katika pointi hii, Roho Mtakatifu anakuwa na kazi ya **kumwezesha** mteule kufanya yale ambayo huko nyuma alikuwa hawezi kuyafanya. **Kolos 1:9-11**

Mfano- Daudi kumuwa simba, dubu na baadaye Goliathi, ni Roho Mtakatifu ndani yake aliyemwezesha **1 Sam 17:32-54**( Roho Mtakatifu **ndiye anayetwezesha hata nasi leo. Gal 2:8**

b. Roho Mtakatifu anafanya kazi kubwa sana ndani yetu ya kutufikisha katika **viwango halisi vya kumjua Yesu Kristo na ukuu wake.**

**Efs 3:17-18, Yoh 16:12-15, Kol 2:1-3**

Hii ya kumjua Yesu Kristo na ukuu wake na uwezo wake siri kubwa naya pekee ambayo bila kujawa na Roho Mtakatifu siyo rahisi ukawa nayo

**Dan 3:15-18!! Kut 14:10-14!! Na hapo ndipo wengi wamekwama;na bila Roho Mtakatifu kutukwamua hapa tutakaa kwenye wokovu kama wenye dini tu!!**

c. Roho Mtakatifu ndiye anatufanya kuwa **watiifu mbele za Bwana**

**Efs 3:19.** Ni Roho Mtakatifu tu anayeweza kuujua upendo wa Kristo unaopita ufahamu wote wa kibinadamu jambo ambalo linatufanya tuwe watiifu mbele za Bwana wakati wote **mfano Mwz 39:6-12** Yusuf kwa sababu aliuja upendo wa ajabu wa Kristo wake; hata saa alipolazimishwa kufanya dhambi hakukubali, au Ayubu saa alipotakiwa kumkufuru Mungu kwa sababu ya mabaya mengi yaliyompata yeye hakufanya hivyo

**Ayub 1:20-22, 2:9-10, 42:7-9**

- **Watimilifu ndiyo waliyo tayari kufa kwa ajili ya imani yao. Ebr 11 yote**

3. Ndiyo sababu leo nasema na Kanisa kwamba; **suluhisho** la mtu wa Mungu la kutopoa kiroho, suluhisho la kuondokana na roho ya woga, suluhisho la kuondokana na tamaa za mwili huu, suluhisho la kuogopa kumshuhudia Yesu mahala popote, suluhisho la kukabiliana na shetani na pepo na waganga wa kienyeji na manabii wa uongo na waalimu wa uongo popote ni kuhakikisha kila wakati **umejawa** na Roho Mtakatifu. **Hata suluhisho la ukame wa maombi ya maombolezo na kuugua toka ndani ya mioyo yetu ni Roho Mtakatifu**

- **Ili tuwe imara bila kutikisika kama Paulo anavyowaambia Wakoritho (1Kor 15:58) lazima wakati wote tuwe tumejawa na Roho Mtakatifu ambaye atatuwezesha kupanda milima yote na kupita mabonde yote bila kuogopa Zab 23:4**

- Ili tufikie katika viwango vya hali ya juu sana ya kumjua Yesu Kristo na ukuu wake kiasi cha kutopeperusha tena na waalimu wa uongo na manabii wa uongo waliojiunga kwa siri katika imani hii **Efs 4:13-14** lazima tujawe na Roho Mtakatifu wakati wote

“ hili ndilo neno la mwisho kabisa la Yesu Kristo kuwaambia na kuwasisitizia sana wanafunzi wake ili walizingatie kama wanataka wawe mashahidi wake popote duniani !! **Mdo 1:8** kwa maana nyingine fupi ni kwamba huwezi kuwa shahidi wa kweli wa Yesu Kristo kama hujajazwa Roho Mtakatifu, utakuwa unapapasa tu na kubangaiza juu ya Yesu Kristo maana ni Roho Mtakatifu tu anayetufanya tumjue Yesu Kristo na ukuu wake kama nilivyofundisha hapo juu

- Tuache mazoea, tuje na kiu ya kumtaka Roho Mtakatifu na Yesu atamwachilia kwa viwango vingine zaidi ndani yetu leo. **Yoh 7:37-39**  
Amina.

**Na**

**Ask Dr. L. Mwizarubi**

**Sept 2021**